



TAARIFA KWA UMMA

HAFLA YA UTOAJI WA VYETI VYA UTHIBITISHO KWA MADEREVA WALIOFAULU MTIHANI NA UZINDUZI WA MITAALA YA MAFUNZO KWA WAHUDUMU WA VYOMBO VYA USAFIRI KIBIASHARA

Kwa mujibu wa Kifungu Na 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, Mamlaka ina jukumu la Kusajili Wahudumu na Kuthibitisha Madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara.

Katika kutekeleza jukumu hilo, tarehe 01 Disemba, 2020 LATRA ilianza kusajili madereva husika na tarehe 01 Juni, 2022 walianza kutahiniwa kwa lengo la kuthibitishwa. Aidha, LATRA kwa kushirikiana na vyuo washirika imekamilisha mitaala itakayotumika kutoa mafunzo kwa wahudumu ili Mamlaka ianze kuwasajili.

Hadi tarehe 31 Mei, 2023 jumla ya madereva 16,332 wamesajiliwa kwenye kanzidata ya LATRA, madereva 1,744 wamejitokeza kufanya mitihani na miongoni mwao wamefaulu na kuthibitishwa. **Mamlaka inawatangazia madereva wote waliothibitishwa kuwa imeandaa hafla ya utoaji wa vyeti ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mhe. Atupele F. Mwakibete (Mb), Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi).**

Hafla hiyo itafanyika Dar es Salaam Jumamosi tarehe 01 Julai, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Arnaoutoglou kuanzia saa 4 (nne) kamili asubuhi. Madereva watakaohudhuria hafla hiyo wanaombwa kuthibitisha ushiriki kwa kutuma ujumbe mfupi wa maandishi wenye jina kamili kama lilivyo katika kitambulisho cha taifa kwenda namba 0734220006 au 0738000090 kabla ya tarehe 28 Juni, 2023.

Imetolewa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano
22 Juni, 2023